BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO, KUSIMAMIA HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Mola Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na viumbe vyote na kutujaalia uhai na uzima na Afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili Tukufu siku ya kwanza ya Mkutano wa Kumi na Nne. Lengo hasa ni kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa mustakbali bora wananchi yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo kwa hakika sisi ni wahitaji kutoka kwake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yetu katika Baraza hili Tukufu katika kuuchangia na kuuboresha mswada huu muhimu katika shughuli za Serikali pamoja na kuhakikisha chombo hiki kimetekeleza jukumu lake la kidemokrasia na kuwa cohmbo chenye ufanisi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa watu wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na afya njema katika kutekeleza majukumu yako ya kutuongoza

vyema na kusimamia hoja zetu za kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa nia njema kabisa inampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji wake mzuri wa majukumu yake ambayo yamepangwa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 – 2025 pamoja na kufanikisha sherehe za kutimimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoleta mabadiliko makubwa katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa maisha marefu na afya njema ili aweze kuitumikia zaidi nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kadhalika, natoa shukurani maalum kwa uongozi mzima wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wakiwemo Waziri, Mheshimiwa Mwl. Haroun Ali Suleiman, Katibu Mkuu, ndugu Mansura Mosi Kassim, Mkurugenzi pamoja na watendaji wote wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kwa ushirikiano wao na juhudi zao kubwa na kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa Mswada huu wa "**Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao, Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo**" ili utekelezaji wake uwe rahisi na wenye ufanisi na tija kwa watendaji na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kwamba, madhumuni na sababu ya kuwasilishwa kwa Mswada huu ni kutunga sheria ambayo itaanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa madhumuni ya usimamizi wa masuala ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma Zanzibar. Ni matumaini ya Kamati yetu kuwa changamoto ambazo zilikuwa zikijitokeza katika Wakala wa Serikali Mtandao zitaweza kutatuka mara tu baada ya Mswada huu kupitishwa na Baraza hili na kuwa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa moyo wa dhati kabisa Wanasheria wetu wa Baraza la Wawakilishi

ambao walikuwa nasi bega kwa bega kuhakikisha Mswada huu unaeleweka ipasavyo. Aidha, pongezi hizi tunazitoa kwa Wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wameutendea haki mswada huu kwa namna walivyoweza kuutengeneza. Bila ya kumsahau mdau wetu kutoka kampuni ya TTCL Zanzibar ambae Kamati yetu ilikutana nae na kupata mashirikiano yake ya kutoa maoni na ushauri wa kisheria kwa lengo la kuimarisha Mswada huu kwa kuzingatia changamoto kadhaa ambazo zinawakabili katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawashauri Wazanzibari kuwa wazalendo na wasichoke kutoa maoni yao pale wanapoona inafaa kwani sote tuna lengo la kuijenga jamii katika utawala bora na kusimamia haki na utawala wa kisheria katika nchi yetu. Sambamba na hilo, Kamati hairidhishwi na kitendo cha baadhi ya wadau ambao hupata mialiko mahsusi kutoka Baraza la Wawakilishi ya kuja kutoa maoni dhidi ya Miswada ambayo inakusudiwa kupitishwa katika Mikutano ya Baraza kwani imekua ni desturi kwa wahusika wengi wanaopatiwa mialiko kutoshiriki kwa kuja na kutoa maoni yao bila ya kutoa sababu za msingi katika za kutohudhuria kwao.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inaitaka jamii kuelewa kwamba mialiko wanayopatiwa lengo lake ni kutumia haki yao kikatiba kwa kutoa maoni na kushirikishwa katika maamuzi. Hivyo, tunashauri kila anaepatiwa mwaliko mbele ya Kamati kufika au kutumia njia mbadala zilizowekwa na Afisi katika kutoa maoni yao, kwani michango yao ni muhimu kwenye utungaji wa sheria ambazo zinatumika katika kujenga mustakbali wa maisha yetu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima na kwa kuthamini michango na ushauri mkubwa katika kutekeleza kazi za Kamati hii, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina Waheshimiwa Wajumbe wanaounda Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyotoa kwa lengo la kufanikisha jukumu hili la msingi kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Mhe. Maryama Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 10. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 11. | Ndg. Shawana Mohammed haji | Katibu, na |
| 12. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora iliupitia na kuujadili Mswada huu siku ya tarehe 06/02/2024 kifungu kwa kifungu na kufahamu malengo na shabaha zilizomo ndani ya Mswada huu, ambapo marekebisho mbali mbali yamependekezwa kufanywa na Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa Sheria hii katika uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kusaidia kupiga hatua kwenye teknolojia ya Habari na mawasiliano ndani ya taasisi za Serikali na zile za binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa uniruhusu kueleza baadhi ya marekebisho na mapendekezo ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika

marekebisho ya Kamati ambayo tayari mmeshapatiwa ili kujisomea kwa ufafanuzi na ufahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Sehemu ya Kwanza kabisa ambayo imeweka ***"Mashari ya Awali"*** katika mswada huu. Kamati inapendekeza kuwekwa sawa mwaka utaoanza kutumika Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa ni mwaka 2024 badala ya mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza juu ya kujenga mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya uratibu, usimamizi na uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA ili kuimarisha utoaji wa huduma za Serikali kwa umma, kwa kuliwezesha hili kamati inaomba kufanya marekebisho madogo katika *Kifungu* Kifungu cha 12 (c) (i) kwa kuingizwa neno **"divisheni"** baina ya neno **"idara"** na **"na"**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuleta ufanisi na utendaji kazi wenye tija na mafanikio ya Mamlaka wa Serikali Mtandao, kupitia Mswada huu, Kamati inapendekeza kurekebishwa kwa kifungu cha 16 ili kuleta usawa wa haki na uwajibikaji wa Mamlaka hii kama ifuatavyo:-

a) Katika kifungu kidogo cha (3), kufutwa maneno **"wakuu wa".**
b) Katika kifungu kidogo cha (4), kufutwa maneno **"na wakuu wa"** na kuwekwa badala yake maneno **"wa vitengo na"**.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati inapendekeza *kifungu cha 18(g)* kurekebishwa kwa kufuta neno "***kuboresha***" na kuandikwa upya neno "***kuimarisha***" kwa ajili ya kuweka maneno sahihi ya kutukia kiswahili sanifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia kifungu cha 25 cha Mswada huu kamati inapendekeza

kurekebishwa kwa neno "***taarifa***" liliopo baina ya neno **"cha"** na **"maana"** na kuwekwa badala yake neno **"data"** ili iweze kuleta maana sawa iliyokusudiwa katika *kifungu cha 2* cha ufafanuzi wa maneno.

**Mheshimiwa Spika,** sote tunafahamu kazi ya kutunga Kanuni ni ya Mheshimiwa Waziri baada ya Sheria kukamilika, hivyo kupitia *kifungu cha 27 (2)* kamati inashauri kufuta maneno **"katika itakavyoainisha na Waziri"** na kuwekwa badala yake maneno "**kama itakavyoainishwa na Waziri katika Kanuni"** ili isije kuleta mkanganyiko wakati wa utungaji wa kanuni utapofika kwa kujua nani ni mtu sahihi wa kutunga kanuni za Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, Kamati yetu inaamini kwamba, kukamilika kwa Mswada huu na kuweza kutumika itakuwa ni msingi bora wa upatikanaji wa ufanisi katika Wakala wa Serikali Mtandao ikiwa dhana pana ya teknolojia ya habari na mawasiliano itazingatiwa kwa umma na utawala bora. Kamati inashauri Mswada huu utakapopita na kuwa Sheria Serikali iendeleze kufanya tafiti mbali mbali zitazokwamua shughuli za mifumo ya TEHAMA inayoleta tija kwa afisi na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu wamepata fursa ya kuupitia kwa kina Mswada huu, na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa ambayo itatoa fursa kwa Wakala wa Serikali Mtandao kuondokana na changamoto zinazowakabili.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu, kwamba Mswada huu ulio mbele yetu waujadili na kuuchangia ipasavyo na hatimae kuupitisha kuwa sheria ikiwa ni sehemu ya jukumu la chombo hiki muhimu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa umakini wao na usikivu wao wa hali ya juu walioonesha wakati nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** *Naomba Kuwasilisha*.

Ahsante,

………………………….

**(Machano Othman Said)**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR**